TAARIFA KWA WANAHABARI KUHUSU UTEKELEZAJI WA AHADI ZA SERIKALI

Imetolewa na Dkt. Hassan Abbasi, Msemaji Mkuu wa Serikali, Dar es Salaam, Januari 8, 2018.

A: SALAAM ZA MWAKA MPYA 2018

- Kwa niaba ya Serikali nianze kwa kuwatakia heri ya mwaka mpya 2018. Katika mwaka huu, kama ilivyokuwa miaka iliyopita, Serikali inaahidi kuendeleza kasi ya mageuzi kwa faida ya Watanzania wote. Niwaombe watumishi wenzangu wote wa umma tuendelee kutoa huduma bora kwa wananchi.

- Katika mageuzi haya wananchi wanaombwa kuendelea kuyaunga mkono kwani ni mageuzi yenye faida kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

SALAAM KWA VYOMBO VYA HABARI

- Katika Mwaka 2018 Serikali itaendelea kushirikiana na vyombo vya habari katika kuripoti mageuzi muhimu yanayoendelea.

- Aidha, tutaanza kutoa “press card” mpya za mwaka huu na pia tukumbuke miaka mitano tuliyopewa kwenda kusoma, inayoyoma, tusijisahau;

- Nawasisitizia endeleeni kutekeleza majukumu yenu kwa weledi mkizingatia misingi ya taaluma hakuna atakayewabughudhi;

Nawakumbusha pia kuwa kuna tuzo mbalimbali za kimataifa mnatakiwa kushiriki (SADC na UNESCO) maelezo ya kina yapo katika www.maelezo.go.tz.

TUZO ZA WANAHABARI 2018

SADC MEDIA AWARDS COMPETITION

TUZO ZA SADC KWA WAANDISHI WA HABARI MWAKA 2018

- **Waandishi wa Magazeti:** Inajumuisha Makala zilizochapishwa katika magazeti,tovuti na ma-jarida.
- **Waandishi wa Redioni:** Inajumuisha vipindi vya utangazaji vya redioni visivyozidi dakika 30
- **Waandishi wa Televisheni:** Inajumuisha vipindi vya utangazaji vya Televisheni visivyozidi dakika 45
- **Wapiga Picha:** Inajumuisha picha kuanzia moja (1) au picha zisizozidi ishirini (20) zilizochapishwa katika toleo moja (pictorial spread) pamoja na maelezo yake (Capitons)

NB: Kazi zote ziwasilishwe Idara ya Habari-MAELEZO kabla ya tarehe 27 Februari, 2018

KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:

ZAMARADI KAWAWA: Baruapepe.: zamaradikawawa@habari.go.tz, Phone: 0754698856

FRANK MVUNGI: Baruapepe.: frank.mvungi@habari.go.tz, Phone: 0652602843

FATMA SALUM: Baruapepe.: fatma.salum@habari.go.tz, Phone:0715651865

TEMBELEA TOVUTI YA: WWW.MAELEZO.GO.TZ

B: HALI YA UCHUMI WA NCHI NA DUNIA

- Kwa maana ya utangulizi tu katika mada yangu ya leo, niseme, katika mwaka 2017 hadi sasa, nchi yetu imeendelea kuwa ya amani na huku uchumi wa nchi yetu ukiwa imara na hata kutajwa kuwa miongoni mwa nchi 5 za Afrika ambazo licha ya mtikisko wa uchumi duniani na Barani humu uchumi wetu bado ni imara na utaendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha kama ripoti zinavyoonesha punde.

Taasisi ya Goldman Sachs ya USA

- Taasisi hii ya wataalamu wa Uchumi ya Marekani inatabiri kuwa wakati uchumi wa dunia mwaka 2018 utakua kwa wastani wa asilimia 4 kutoka 3.7 mwaka jana, Tanzania itakua na ukuaji wa juu usiopungua asilimia 6.5.

- Haya yamo katika ripoti yao iitwayo **"2018 Global Economic Outlook-As Good As It Gets."** ya Novemba 15, 2017.

-

Ripoti ya UN Kuhusu Uchumi 2018

- Nayo Ripoti ya UN iitwayo "World Economic Situation and Prospects 2018" ya mwaka huu inatabiri kuwa uchumi wa dunia hautakuwa na ukuaji wa chini ya asilimia 3.0.

- Ripoti hiyo inaioredhesha Tanzania kuwa miongoni mwa nchi 5 za Afrika ambazo uchumi wake utakua kwa kasi ya kufikia asilimia 6.8.

- Sisi uchambuzi wetu na lengo letu kama nchi bado ni kukua kwa asilimia 7.0 na lengo ni kuvuka zaidi ya hapo.

Ripoti ya IMF Kuhusu Uchumi 2018

- Kama ilivyo kwa Ripoti ya UN, Ripoti ya Shirika la Fedha Duniani (IMF) ya Oktoba, 2017 **"World Economic Outlook October, 2017"** ikionesha matarajio ya Uchumi katika mwaka 2018 inaonesha Tanzania ikiwa miongoni mwa nchi chache za Afrika ambazo uchumi wake utakua kwa kasi kama ifuatavyo:

- Ethiopia (8.5), Kodivaa (7.3), Senegal (7.0), Tanzania (6.8) na Kenya (5.5).

Mwaka 2017 Tulikuwa 10 ya Dunia kwa Ukuaji wa Uchumi

The world's fastest growing economies

Forecast GDP growth, 2017

WORLD ECONOMIC FORUM
COMMITTED TO IMPROVING THE STATE OF THE WORLD



Source: World Bank

B:KUTOKA “UCHUMI MKUU” HADI “UCHUMI WA WATU”; UTEKELEZAJI WA AHADI

UTANGULIZI

- Shule kuu mbili za fikra katika uchumi zinasisitiza kuwa ukuaji wa uchumi unaweza kutazamwa kwa takwimu pana **(quantitative levels)** au katika mawanda ya namna ukuaji wa uchumi unavyoakisiwa kupitia maendeleo ya jamii **(qualitative levels).**

- Serikali ya Tanzania inaamini katika shule zote hizo mbili za fikra-kwamba ni muhimu uchumi wetu kukua vyema katika takwimu pana, lakini ni vyema hali hiyo ijidhihirishe pia katika kuinua maisha ya jamii. Lakini pia nidhamu katika kuahidi na kutekeleza vimeleta mafanikio tunayoyataja leo.

1.AHADI YA KUHAMIA DODOMA

…SERIKALI TAYARI IKO DODOMA

- TUMETEKELEZA: Kama nilivyoeleza mara ya mwisho, Viongozi wote Wakuu wameshahamia Dodoma.Kwa sasa ni Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pekee anayesubiriwa kuhamia wakati wowote mwaka huu.

- Mpaka kufikia Januari mwaka huu, jumla ya wafanyakazi **waliohamia Dodoma ni 3,671** na **awamu inayofuata watahamia wengine 2,460.**

- Niiombe sekta binafsi ikachangamkie fursa zilizopo Dodoma kwani suala la kuhamia halina tashtiti tena. Linakamilika.

2.UTEKELEZAJI SERA YA VIWANDA

- Moja ya ajenda kubwa na ambayo mara kwa mara hapa tutakuwa tunaitolea maendeleo yake ni sera ya kuhamasisha na kuvutia wawekezaji katika sekta ya viwanda.

- Hii ni kwa sababu tunaamini kuwa sekta ya viwanda-kuanzia vidogo, vya kati hadi vikubwa ina manufaa anuai kwa uchumi kuanzia kusaidia teknolojia, ajira na kukuza sekta nyingine kama kilimo na miundombinu.

TAKWIMU ZA SEKTA YA VIWANDA

- Hadi kufikia robo ya mwisho ya mwaka 2017, tumesajili miradi ya zaidi ya viwanda 3,300, kati ya hiyo kuna viwanda vikubwa 652 vyenye jumla ya mtaji wa zaidi ya TZS trilioni 5 inayotarajiwa kuajiri **watu 50,625.** Usajili ni kama ifuatavyo na baadhi ya viwanda hivi vimeanza kufanyakazi:

- 1.TIC miradi 361;
- 2.EPZ miradi 41;
- 3.BRELA miradi 250; na
- 4.SIDO viwanda vidogo 2,721 vinavyoajiri watu kuanzia mmoja hadi 9.

KIWANDA KIPYA CHA SAYONA MWANZA

Matreka ya Ursus 727 Yameunganishwa Kibaha, TZ

KIWANDA KIKUBWA CHA VIGAE KUSINI MWA SAHARA

Tanzania Tile Factory

Investment:
USD100m

Production:
800,000 tiles
per day

Employment:
1,500 Tanzanians
Directly Employed

Distribution:
Tanzania, Kenya,
Burundi, Uganda, Rwanda

KIWANDA KIDOGO CHA KUSINDIKA VITUNGUU SAUMU, MBULU.

KIWANDA KIDOGO CHA VITUNGUU

MKOA WA
SIMIYU-TUNATEKELEZA
WHITE
DUSTLESS
SCHOOL CHALKS

3.UZALISHAJI WA UMEME KINYEREZI

- **1.Kinyerezi-1 extension**: Megawati 185 uko katika asilimia 50 kukamilika. Ni mradi wa USD milioni 188. Mradi huu unatekelezwa kwa 100% fedha ya Serikali.

- **2.Kinyerezi II**: Megawati 240 mradi wa USD milioni 354.6 uko asilimia 87 lakini kati ya Desemba 8 na 9, 2017 **megawat 55.94** zimeingia katika grid. Megawat nyingine 27 zitaingia katika gridi kabla ya mwisho wa Januari hii. Miradi yote hii itakamilika mwaka huu. Mradi huu unatekelezwa kwa kushirikiana na Serikali ya Japan.

4.UJENZI WA RELI YA KISASA "STANDARD GAUGE"

- Ujenzi wa reli ya kisasa (Standard Gauge) kwa kipande cha Dar-Morogoro kilometa 300 ikijumuisha ujenzi wa kilometa 205 njia kuu na kilometa 95 ikiwa ni njia za kupishana treni, ujenzi unaendelea kwa kasi tangu ulipozinduliwa April, 2017. Kipande hiki kitagharimu TZS trilioni 2.7.

- Usanifu wa njia yote itakayopita reli umekamilika kwa asilimia 100 na tathmini ya fidia imekamilika kwa asilimia 75 huku ujenzi wa tuta na madaraja madogo ukiendelea.

5.UNUNUZI WA TRENI YA KISASA YA UMEME

Wakati ujenzi wa reli ukiendelea, Serikali imeshatangaza zabuni kwa ajili ya kupata makampuni yatakayopewa tenda ya kutengeneza vichwa na mabehewa ya kisasa ya treni ya umeme na ya kawaida. Zabuni zitafunguliwa Januari 31, 2018.

Katika zabuni hiyo kuna vichwa 25, mitambo mingine zaidi ya 25 ya ukarabati wa reli na mabehewa 1,590 (kati ya hayo 1,530 yakiwa ni ya aina mbalimbali za mizigo kama vile makontena, mafuta n.k na 60 ni ya abiria (15 yakiwa ni VIP coach).

Reading

3827
3827
QRNational

Double Stack Container Wagons 50

Oil Tankers 200

6.MELI ZA KISASA KATIKA MAZIWA

- Serikali pia imeanza kutengeneza meli za kisasa ili kuondoa adha ya usafiri katika maziwa makuu:

- **1.ZIWA NYASA:** Juzi meli mbili mpya za mizigo za MV Njombe na MV Ruvuma ambazo zinabeba tani 1,000 za mizigo kila moja na zimetumika TZS Bilioni 11.252 zimeanza kufanya safari rasmi. Meli ya abiria itakayobeba watu 200 na mizigo tani 300 itakamilika Juni mwaka huu.

- **2.ZIWA VICTORIA:** Meli mpya kubwa 2 mkandarasi ashapatikana zitatengenezwa ndani ya mwaka mmoja ila **MV Clarios ya abiria** na **MV Umoja** ya mizigo zimekarabatiwa na zimeanza kazi chini ya kazi nzuri ya kampuni ya Serikali iitwayo “Marine Services Company LTD.”

ASANTENI SANA

@MAELEZO 2018